OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA NKASI

SHULE YA SEKONDARIKIPILI,
S.L.P 127,
NAMANYERE-NKASI.
TAREHE 08/12/2019
MOB: 0765521845
0769061781
0768168138

KUMBU: NA. _____

MWANAFUNZI_____

S.L.P _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIPILI
MWAKA 2021

Ninafurahi kukuarifu kuwa umewchaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Kipili kidato cha kwanza mwaka 2021 shule ipo umbali wa Km 67 maghalibi mwa mji Mkuu wa Wilaya ya Nkasi (Namanyere). usafiri wa mabasi unapatikana kutoka mjini Namanyere kwa nauli ya Tsh.5000/=

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 Hivyo unatakiwa kuripoti tarehe 11/01/2021 bila kukosa.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A) **SARE YA SHULE (WASICHANA)**
-Sketi mbili, nyeusi na nyekundu damu ya mzee kitambaa kizito (mshono linda box sketi ndefu ya kisasa)
-Shati mbili nyeupe mikono mifupi
-Soksi nyeupe pea mbili
-Skafu mbili nyeusi na nyekundu damu ya mzee
-Viatu vyeusi soli fupi pea mbili
-Vifaa vya michezo (tisheti ya njano, sketi ya bluu, soksi za bluu na raba)

B) **SALE YA SHULE WAVULANA**
-Suruali mbili nyeusi na nyekundu damu ya mzee kitambaa kizito

-Shati mbili nyeupe mikono mifupi
-Soksi nyeupe pea mbili
- Viatu vyeusi soli fupi vya kufunga kamba visivyo vya mchongoko pea mbili Tai nyeusi mbili
- Vifaa vya michezo (tisheti ya njano bukta ya bluu soksi ndefu za bluu na raba)

NB Kwa waislamu rangi ya hijabu ifanane na sare za shule .

C) SARE YA HOSTEL.

- **WASICHANA:** Gauni lililoshonwa kimaadili rangi ya bluu bahari kitambaa kizito pea mbili.

D.) UBORESHAJI NA USAFI WA MAZINGIRA

i. Kila mwanafunzi aje na miche (3) ya miti ya matunda kwa ajili ya kupanda.
ii. Mwanafunzi aje na jembe moja lenye mpini , fyekeo na ndoo ya lita (10)

E) VIFAA VYA MALAZI NA BWENI

i. Godoro jipya single imara
ii. Shuka mbili nzito rangi ya bluu bahari (wavulana) wasichana rangi ya pink
iii. Mto/Pillow folonya ya bluu bahari (wavulana) wasichana rangi ya pink.
iv. Msengele mmoja kutanguliza kitandani kabla ya godoro
v. Sanduku imara la bati/mbao la kutunzia vifaa.
vi. Dumu la lita 5 la kutunzia maji ya kunywa.
vii. Ndoo mbili za lita 10 za kufanyia usafi.
viii. Sabuni za kutosha kuogea na kufulia
ix. Kanda mbili za viwandani kwa ajili ya kuogewa
x. Taulo kwa ajili ya kuogea
xi. Chandarua moja(01)

F.) VIFAA VYA KITAALUMA

i. Daftari za kustosha size kubwa
ii. Biki za kutosha
iii. Mkebe mpya wenye vifaa vyote
iv Kamusi /Dictionary kwa ajili ya Kiswahili/Kiingereza

G.) MICHANGO YA CHAKULA

i. Mahindi debe 10 kwa mwaka , nusu mwaka debe 5
ii. Maharage debe 3 kwa mwaka nusu mwaka debe 1 na nusu
iii. Fedha za upishi Tsh. 60,000/= nusu mwaka Tsh. 30,000/=

NB: Mwanafunzi atapokelewa endapo atakuwa na kianzio cha mahindi debe 04 maharage debe 1 na nusu au fedha Tsh. 30,000/=

Aidha aje na vyombo vya chakula ambavyo ni sahani moja ya self contena (yenye schemu tatu) va bati au plastic gumu, kiiiko na kikombe kimoja cha musi lita kwa aiili ya matumizi ya kunywa

H) ANGALIZO KWA WANAOKAA HOSTEL

Ifahamike kuwa mwanafunzi yeyote mwenye tatizo au ugonjwa wowote unaoibuka ghafla na kuhitaji uangalizi maalumu MI Kifafa, kizunguzungu, kuanguka kupoteza fahamu na mengineyo ya kienyej, inashauriwa akae kijijini kwa ndugu au jamaa ili aweze kuhudumiwa na kupata msaada unaotakiwa kwa wakati.

Taratibu za shule haziruhusu wanafunzi wanamna hiyo kukaa Hosteli.

NB: Endapo mwanafunzi mwenye matatizo hayo atabainika Hosteli taratibu zitafuatwa.

I) SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa umakini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hivyo wakati wote wa wanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma

J) MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji

4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi cocaine, mirungi na kubeli na kadhalika
5. Kupiga au kupigwa
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba/kumpa msichana ujauzito
9. Kutoa mimba
10. Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvunga amani na usalama wa shule au watu.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi
12. kuwa na simu ya mkononi
13. Kukutwa au kuonekana kwenye baa au kumbi za sterehe

K) MAMBO MENGINE YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine ya shule

NB: Fomu za afya na mikataba vitarejeshwa shuleni mwanafunzi anapokuja kuripoti.

Tafadhali zingatia maelekezo yote uliyopewa katika fomu hii ili kuepusha usumbufu usio wa lazima

Nimakutakia maandalizi mema na ninakukaribisha sana Kipili Sekondari.

.....

J.B. KASANYI
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
KIPILI SECONDARY
NKASI

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA NKASI
SHULE YA SEKONDARI KIPILI

FOMU YA MKATABA KATI YA MZAZI KWAAJILI YA KUJIUNGA NA SHULE SEKONDARI KIPILI

A) MWANAFUNZI

Mimi _____ninakubali/sikubali kujiunga na shule ya sekondari Kipili na kwmaba nitasoma mpaka kidato cha nne. Aidha nikotayari kufuata sheria kanuni na taratibu zote za shule na za kuishi Hostel endapo nitakaa Hostel. Pia nimesoma maelekezo na maagizo yote ya kujiunga na shule na nitatekeleza.

NB: Endapo nitaenda kinyume na taratibu au sheria za kukaa hosteli nitakuwa tayari kupokea adhabu ikiwa ni pamoja na kuondolewa Hostel.

SAHIHI YA MWANAFUNZI_____

B) MZAZI/MLEZI

Mimi_____ Mzazi/mlezi wa_____ ninakubali mwanangu asome shule ya sekondari kipili na nitamsimamia mwanangu kuzifuata taratibu zote za shule. Pia nikotayari kutekeleza maagizo na maelekezo yote ya kujiunga na shule ya sekondari Kipili.

NB: Endapo mwanangu atakaa Hosteli naikatokea amekwenda kinyume na sheria na taratibu za kukaa Hosteli nitaunga mkono mwanangu kupewa adhabu na hata kuondolewa Hostel.

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI _____

TO BE COMPLETED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER AND TO BE RETURNED TO THE HEADMASTER KIPILI SECONDARY SCHOOL

REF .....

Please examine named above and comment his her health responding to the following items kindly

Put tick in front of either YES or NO

Does the student have problem in connection with

A, Sight? ..... NO/YES

If yes

state .....

B, Hearing? ..... NO/YES

If yes

state .....

C, Speech? ..... NO/YES

If yes

state .....

D,T.B? ..... NO/YES

If yes

state .....

E, Blood Pressure? ..... NO/YES

If yes

state .....

F, Any physical disability? ..... NO, YES

G; Any other health problem? ..... NO/YES

If yes

state .....

Do you therefore recommended the student to be physically fit for admission in this school?

1 YES

2. NO

If NO state reason

.....

.....

.....

.....

Name and Signature

Date .....

Designation

Stamp

MKATABA NA MASHARTI KWA WANAFUNZI WANAOKAA KATIKA HOSTEL YA SHULE YA SEKONDARI KIPILI

Yafuatayo ni masharti na maelekezo maalumu kwa mwanafunzi yeyote atakaye hiari kuja kukaa hostel, endapo atakikuka mojawapo, ataondolewa hostel mara moja na kutafuta mahala pengine pakukaa.

(i) Kuchangia michango ya chakula kwa wakati na si chini ya nusu ya mchango husika kwa muhula.

(ii) Kuwa na vifaa kamilifu vya malazi yaani Godoro imara, shuka 2 bluu bahari(wavulana) rangi ya pinki (wasichana), msengele na mto

(iii) Kujiepusha na ulevi, wizi, uzinzi, ugomvi, madawa ya kulevya, kuchorachora na kuweka maandishi ukutani, migomo na tabia zisizofaa.

(iv) Kutii na kufuata taratibu, kanuni na ratiba ya shule kuanzia muda wa kuamka mpaka muda wa kulala.

(v) Kujiepusha na maneno au vitendo vyovyote vinavyoweza kuhatarisha amani na utulivu wa shule.

(vi) Kuomba ruhusa unapokuwa na sinda ya kuondoka shuleni na kurejea kabla ya saa 12:00 Alasiri.

(vii) Kushiriki bila kutega katika kazi mbalimbali za usafi wa bweni, mazingira ya nje na nyinginezo.

(viii) Kuepuka uharibifu wa mali na samani za umma kama vile vitanda, viti, madawati, milango, madirisha n.k.

(ix) Kuepuka kuweka bwenini vitu vyote vinavyoweza kuzua moto mf.kiberiti, pasi, mshumaa, koroboi, taa ya mafuta n.k (usijenavyo kabisa hapa shuleni)

(x) Wenye matatizo maalum na magonjwa ya asili inashauriwa wakae kwa uangu au jamaa zao kijijini.

Nimeyasoma na kuyaelewa masharti na maelekezo yote yaliyomo katika fomu na mkataba huu.

Na hivyo basi nakubali/sikubali (Hutaisiyotakiwa) kuyatii na kuyatekeleza.

1. JINA LA MWANAFUNZI .....
   SAHIHI .....
2. JINA LA MZAZI/MLEZI.....
   SAHIHI .....